

**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI**

*(Chini ya Sheria Nc. 4 ya 2010)*



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UUZAJI  
WA MICHORO YA MAJENGO**

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi(AQRB) inatoa onyo kwa watu wanaochora na kuuza ramani/michoro ya Ubunifu Majengo na kusambaza katika **Vitabu, Majarida** katika maeneo ya **Barabara, Mitandao Ya Jamii** kama **Facebook, Instagram**,n.k hapa Dar es Salaam na mikoa mingine.

Aidha, Bodi inatoa **Tahadhari** kwa wananchi wote kutonunua au kutotumia Michoro hiyo ambayo imeandaliwa na watu wasioajiliwa na wasiotambulika kisheria. Hivyo huduma wanazotoa kutokuwa na viwango vinavyohibitika. Kutuma michoro hiyo siyo tu ni kinyume na Sheria bali pia kunaweza kuleta madhara katika matumizi yake.

Ikumbukwe kuwa michoro ya ujenzi wa majengo hufanywa na Mbunifu Majengo, kupitia makampuni ya iyosajiliwa kisheria ili kuhakikisha inakidhi viwango vya ujenzi wa jengo husika, kwa kuzingatia matumizi mbalimbali ya eneo husika.Hili hufanyika kwa weledi na kufuata maadili ya taaluma.

Ifahamike kuwa si kila ramani ya jengo inafaa katika kila eneo la ujenzi kwani kila eneo la ujenzi lina mazingira tofauti; kwa mfano hali ya hewa, miundo mbinu iliyopo, hali ya ardhi, aina ya udongo, matumizi ya jengo n.k. kwa maana hiyo tunasisitiza katika

kutafuta ramani za majengo wananchi wawatumie **Wataalamu waliosajiliwa na Bodi** watakaoweza kubuni michoro inayoendana na mazingira ya eneo husika na gharama halisi ya jengo.

Aidha, Bodi inawataka watu wote wanaojihusisha na **Kuchora na Kuuza Ramani Za Majengo Kinyume Na Sheria Kuacha Mara Moja**, na endapo watakaidi onyo hili, **BODI** itawachukulia hatua kali za kisheria, ikiwemo **faini** isiyo chini ya **shs 5,000,000.00** au **kifungo** kisichopungua cha **miaka mitatu** au vyote kwa pamoja kwa muftu wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriji Majenzi Na. 4 ya 2010.

Imetolewa na Msajili  
Bodi ya Usajili wa  
Wabunifu Majengo na Wakadiriji Majenzi  
S.L.P Box 72673 Dar Es Salaam  
Simu: 2110292  
Nukshi: 2117535  
Barua Pepe: [info@aqrb.go.tz](mailto:info@aqrb.go.tz)  
Tovuti: [www.acrb.go.tz](http://www.acrb.go.tz)